Tangazo La Serikali Na. 671 la tarehe 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA KAWAJENSE YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Kawajense ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda.

______

JEDWALI

______

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Mpango wa Urasimishaji lipo ndani ya Mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mipaka ya upimaji namba 'B1' yenye majira - nukta 287667E, 9299821N kuanzia barabara ya Mikocheni kwenda unaelekea Kusini - Magharibi uelekeo wa S 05°29'34"W kwa umbali wa kilomita 0.193 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba B2 yenye majira - nukta 287649 E, 9299629 N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi uelekeo wa S 36°23'49"W kwa umbali wa kilomita 0.109 B3 yenye majira - nukta 287540 E 9299622 N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi uelekeo wa S 06°45'10"W kwa umbali 0.034 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba B4 yenye majira – nukta 287536 E 9299588 N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi uelekeo wa S 83°34'18"W kwa umbali wa kilomita 0.214 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba B5 yenye majira - nukta 287272E,9299618N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi uelekeo wa S 26°35'07"W umbali wa kilomita 0.029 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba B6 yenye majira - nukta 287259 E, 9299592 N, S 45°48'02"W umbali wa kilomita 0.053 B7 yenye majira - nukta 287221 E, 9299629 N, S86°35'58"W kwa umbali wa kilomita 0.324 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba B8 yenye majira - nukta 286898 E, 9299610 N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki uelekeo wa N 10°35'56"E kwa umbali wa kilomita 0.072 B9 yenye majita – nukta 286911 E, 9299680 N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi uelekeo wa N00°55'44"W umbali wa kilomita 0.201 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba B10 yenye majira - nukta 286908 E 9299881 N) baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki uelekeo wa N 88°11'23"E kwa umbali wa kilomita 0.251 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba B11 yenye majira - nukta 287160 E, 9299889 N) N 13°49'23"E kwa umbali wa kilomita 0.067 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba B12 yenye majira - nukta 287175 E, 9299954 N, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki uelekeo wa S 74°54'54"E kando ya barabara ya Mikocheni kwa umbali wa kilomita 0.509 hadi ilipoanzia alama ya mpaka ya upimaji namba B1 yenye majira - nukta 287667 E 9299821 N."

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*